Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu

Elimu Kwa Wazazi, Walezi Na Walimu Kuhusu Usalama Wa Mtoto Mtandaoni.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum
Mji wa Serikali - Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 573,
40478 DODOMA.

Simu: +255 (26) 2963341/2963346
Fax: +255 (26) 29634348
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz
Tovuti: www.jamii.go.tz

Oktoba, 2022

Yaliyomo

Dibaji.....ii

Tafsiri ya maneno.....iii

Kwa nini unapaswa kuzungumza na watoto kuhusu matumizi ya mtandao?.....1

Kitu gani unapaswa kuzungumza na watoto: Aina za ukatili dhidi ya watoto mtandaoni.....2

Uraibu wa mtandao.....5

Ni nani anafanya ukatili na unyanyasaji wa kingono kwa watoto mtandaoni?.....6

Madhara ya ukatili na unyanyasaji wa kingono kwa mtoto.....7

Wazazi na walezi wanaweza kufanya nini kusaidia watoto?.....8

Walimu wanaweza kufanya nini kusaidia watoto?.....12

Vyanzo vya taarifa.....15

Dibaji

Utafiti wa ***Disrupting Harm*** kuhusu hali ya ukatili dhidi ya watoto mtandaoni unaeleza kwamba karibu asilimia 4 ya wasichana na wavulana wanaotumia mtandao nchini Tanzania wanafanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kingono mtandaoni. Hii inamaanisha watoto wanalazimishwa kushiriki katika shughuli za kingono mtandaoni. Shughuli hizi ni pale ambapo mtu mwingine anatoa au anaweka picha za ngono mtandaoni bila ruhusa yao, au ambapo wanashinikizwa kushiriki ngono kwa ahadi za kupewa pesa au zawadi. Ikilinganishwa na idadi ya watu wa Tanzania, hii inawakilisha wastani wa watoto 200,000 wenye umri wa miaka 12 mpaka 17. Kadiri matumizi ya teknolojia ya simu yanavyozidi kuongezeka, idadi hii inatarajiwa kuongezeka zaidi.

Hivi sasa watoto wanatumia mtandao kwa wingi zaidi kuliko hapo awali. Matumizi haya yanawafungulia fursa mpya, lakini pia yanawaweka kwenye uwezekano wa hatari ya kupata madhara. Je, ni kwa jinsi gani wazazi au walezi na walimu wanaweza kuhakikisha kwamba, watoto wanapotumia vyombo vya kidijiti wameandaliwa kudhibiti madhara yanayoweza kuwatokea. Tambua kwamba udhibiti uendane na ruhusa ya kuwawezesha watoto kupata manufaa yanayotolewa na teknolojia ya mtandao.

Kitini hiki kinatarajiwa kujenga ufahamu na kutoa maarifa juu ya ukatili na unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto mtandaoni kwa wazazi, walezi na walimu; kuwapa taarifa muhimu na vidokezo vya kuwalinda watoto mtandaoni na kuwajulisha usaidizi na njia za kutoa taarifa za ukatili na unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto mtandaoni.

Dkt. Zainab A.S Chaula
Katibu Mkuu

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

TAFSIRI YA MANENO

Arafa – Ujumbe mfupi wa maandishi.

Dhuru – Kusababisha maumivu au majeraha ya mwili au akili au sifa za mtu kwa njia yoyote ile.

Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto - Kitengo maalum ndani ya Jeshi la Polisi Tanzania chenye askari waliohitimu mafunzo maalum ya kushughulikia kesi za ukatili dhidi ya watoto na unyanyasaji wa kijinsia.

Kidijiti - Teknolojia ya kielektroniki inayozalisha, kuhifadhi na kuchakata data.

Mitandao ya kijamii - Programu tumizi za kompyuta zinazoruhusu watu kuwasiliana na kupeana taarifa kwenye mtandao kwa kutumia kifaa cha kielektroniki kama vile kompyuta au simu ya mkononi. Mfano wa mitandao ya kijamii ni Facebook, Twitter, Instagram na WhatsApp.

Mawasiliano mtandaoni – njia za mawasiliano ambayo ni ya kielektroniki.

Mhalifu mtandaoni - Mtu anayefuatilia watu mtandaoni kwa lengo la kuwadhuru au kufanya uhalifu dhidi yao.

Mtandao – Kuunganishwa kwenye intaneti ili kuweza kutumia huduma za mtandao.

Nywila – Neno la siri

TEHAMA - Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Huu ni mchanganyiko wa teknolojia ya habari, utangazaji na mawasiliano.

Uraibu – Hali ya mazoea yaliyopitiliza katika kufanya kitu au utumiaji wa kitu flani ambao unaleta madhara kwa mtu kama kutumia intaneti kila mara.

Utambulisho - jina la mtu na taarifa ambazo zinamtambulisha.

Kwa nini unapaswa kuzungumza na watoto kuhusu matumizi ya mtandao?

Mtandao huwezesha watoto kujifunza, kuvumbua, kuwa wabunifu na kuwasiliana na wengine. Hii inawaweka kwenye hatari kubwa ya kupata madhara ya ukatili. Hata kama tutawakataza watoto kutumia mtandao au kutunga sheria kali, bado watoto wana uwezo wa kupata njia mbadala ya kuingia mtandaoni. Unapochukua tahadhari za kuwalinda watoto dhidi ya madhara ya ukatili mtandaoni, unamlinda mtoto wako dhidi ya madhara na shughuli zinazoweza kumhatarisha au zisizofaa mtandaoni. Unapomfundisha mtoto wako jinsi ya kutambua hatari na hatua za usalama za kuchukua, unakuwa unaongeza uwezo wa mtoto wako wa kukabiliana na hatari zote anazokabiliana nazo mtandaoni. Mtandao hutoa fursa kwa watoto kupata maarifa mapya, kupata masuala ya kijamii na kisiasa, na kushiriki katika maisha ya kiraia. Mtandao ukitumika ipasavyo, watoto wanaweza kufurahia manufaa na fursa mbalimbali zinazotokana na mtandao.

Kitu gani unapaswa kuzungumza na watoto: Aina za ukatili dhidi ya watoto mtandaoni

Sisi wazazi, walezi na walimu, tunapaswa kuwahimiza watoto wetu matumizi sahihi ili waweze kunufaika na fursa zilizopo mtandaoni. Aidha, tuwaweke wazi kwa kuwaeleza kwamba katika matumizi ya mitandao hiyo wanaweza kukabiliana na aina tofauti za ukatili na unyanyasaji wa kingono. Zifuatazo ni baadhi ya aina za ukatili na unyanyasaji wa kingono mtandaoni ambazo mtoto anapaswa kuzifahamu.

Nyenzo za udhalilishaji watoto kingono. Hizi ni picha, video, vitabu vya katuni, katuni na vingine vingi vinavyo onyesha sehemu za siri za mtoto au watoto wakinyanyaswa kingono.

Udhalilishaji na vitisho kwa kutumia picha. Hii inamaanisha kulazimisha mtu kutuma picha na video chafu kisha kuzitumia dhidi yake. Mara nyingi waathirika wa hili hutishiwa kwamba wasipofanya ngono, kutoa pesa au kufanya mambo mengine na hao watu wanaotaka wafanye hivyo basi picha zao zitawekwa hadharani mtandaoni au kwenye mitando ya kijamii.

Kumrubuni mtoto mtandaoni.

Hii inamaanisha kujenga uhusiano na mtoto kupitia mtandao kwa lengo la kumdhalilisha kingono.

Meseji za ngono. Hii inamaanisha kutuma au kupokea ujumbe wa maandishi, picha au video zenye maudhui ya kingono kutoka kwa watu wanaojulikana au wasiojulikana kwa lengo la kukushawishi kufanya ngono.

Udhalilishaji kingono mbashara. Hii ni pale mtoto anapolazimika kuchukuliwa video za ngono ama akiwa peke yake au na watu wengine. Wakati huo huo, video hii hupitishwa moja kwa moja mtandaoni na kutazamwa na wengine katika maeneo tofauti.

Uonevu mtandaoni ni pale mtu binafsi au kikundi cha watu kinapoamua kumwaibisha, kumfedhehesha, kumtishia, kumtusi au kumdhalilisha mtoto kupitia arafa za simu, mitandao ya kijamii au aina nyingine za mawasiliano ya kielektroniki. Hapa chini unaweza kupata baadhi ya mifano ya uonevu mtandaoni:

- Kutuma ujumbe mbaya au wa vitisho mtandaoni kuhusu mtoto
- Kueneza uvumi mtandaoni ili kuharibu sifa ya mtoto mwingine
- Kuiba akaunti ya mtandao ya mtoto mwingine na kuitumia kutuma ujumbe, picha au video za kuumiza
- Kuunda akaunti mtandaoni ambazo zina hadithi, katuni, picha au vichekesho vinavyodhalilisha watoto wengine
- Kupiga na kuweka picha ya aibu ya mtoto mwingine au rafiki mtandaoni
- Kumdanganya mtoto mwingine au rafiki kwa lengo la kutoa habari zake binafsi na kuzisambaza kwa wengine
- Kuchapisha taarifa za kuumiza au za uongo kuhusu mtoto au mtu mwingine mtandaoni
- Kuhariri na kuweka picha za watoto wengine mtandaoni

Kwa kuwa watu katika jamii wanatembea na simu zao za mkononi, saa janja na vifaa vingine vya kielektroniki ni rahisi kwao kumfikia mtoto na kumrekodi mahudhui ya kingono na hatimaye kuyafikisha mtandaoni. Ni muhimu kwa wazazi, walezi na walimu kujua kwamba unyanyasaji mtandaoni unaweza kumfuata mtoto kila mahali, hata katika maeneo salama na ya faragha kama vile nyumbani, shuleni, kwenye basi la shule, kanisani au msikitini na wakati wa michezo.

Uraibu wa Mtandao

Pamoja na faida zilizopo mtandaoni kwa watoto wetu, mtandao pia unaweza kulevya na kuleta uraibu. Fursa na hamasa zinazoletwa na mtandao zimesababisha baadhi ya watoto kujikuta wanakaa muda mrefu kwenye mtandao. Ili kumtambua mtoto anaetumia mtandao kupita kiasi unaweza kuangalia tabia na mienendo yao kama zifuatazo.

- Mtoto anapoanza kujisikia vizuri zaidi na kutumia muda mwingi kuwa na marafiki mtandaoni kuliko wanafamilia na marafiki nje ya mtandao.
- Pale mtoto anapokuwa hawezi kuacha au kupunguza muda unaotumika kwenye shughuli za mtandaoni kama vile kucheza michezo, kupakua programu au kutazama video mtandaoni.
- Mtoto anapotoroka shuleni au shughuli za kila siku lakini kupata muda wa kuvinjari mtandaoni.
- Mtoto anapoachana na mambo muhimu kama vile kazi za nyumbani, kazi za kila siku, kula chakula kwa wakati na kulala ili kutumia muda mtandaoni.
- Mtoto anapokuwa na hali ya huzuni au kuudhika anapokatazwa au kuombwa kuacha kutumia mtandao au vifaa vinavyotumika kupata mtandao.
- Mtoto anapotumia mtandao kuepuka matatizo kama vile kutokuwa na furaha, huzuni na woga.
- Mtoto anapokiuka utaratibu wa familia wa matumizi ya vifaa vya kieloktroniki nyumbani kwa kuiba na kudanganya muda unaotumika mtandaoni.

Ni nani anafanya ukatili na unyanyasaji wa kingono kwa watoto mtandaoni?

Mtu yeyote, mwanamume au mwanamke, kutoka popote katika sehemu mbalimbali za dunia, wakiwemo wanafamilia, wanaweza kuwa wahusika wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto mtandaoni. Tafiti mbalimbai zilizofanyika hapa nchini zinaonesha kwamba wahusika ni watu walio jirani na watoto au wanaowafahamu. Watu hawa ni kama watoto wenzao, marafiki, jamaa, wazazi, walimu, wahudumu wa nyumbani, wa kike au wa kiume. Uhalifu huu hutokea pale watoto wanapokuwa mtandaoni au ana kwaana. Mitandao ya kijamii kama vile, Facebook, Instagram na WhatsApp ndio majukwaa ya kawaida ambapo watoto hupitia ukatili na unyanyasaji wakingono nchini Tanzania.

> "Akaunti yangu ya Facebook inaitwa (jina limefichwa). Niliifungua mwaka jana na ilikuwa na marafiki 100 pekee.Lakini siku zilivyozidi kwenda, sijui watu waliionaje, na sasa nina marafiki zaidi ya 4,337 kwenye Facebook. Bado sijui jinsi watu wanavyoichukulia akaunti yangu. Watu wengine wanafikiri mimi ni shoga na wanatuma picha chafu na maneno ya kuumiza ambayo sikuwahi kufikiria maishani mwangu. Kwa mfano, mtu anasema kitu kama "nakupenda", "Nataka uwe mke wangu" huku ukijua wewe ni mvulana. Mbaya zaidi anakutumia picha zake za utupu na kukuomba utoe za kwako".
>
> **(Ushuhuda wa mtoto wa Kitanzania wa miaka 14).**

Madhara ya ukatili na unyanyasaji wa kingono kwa mtoto

Kama ilivyo ukatili na unyanyasaji wa kingono kwa watoto unaofanyika nje ya mtandao, ukatili wa mtandaoni pia una madhara makubwa ya muda mrefu ya kimwili, kisaikolojia, kijamii, kitaaluma na kiafya kwa watoto na vijana. Zifuatazo ni baadhi ya athari za ukatili na unyanyasaji wa kingono kwa watoto mtandaoni:

Athari za kisaikolojia. Hii inahusisha kuvunjwa moyo, kupata mfadhaiko, woga, upweke, huzuni, wasiwasi, mawazo ya kujiua, kutojistahi, kutokuwa na uwezo, kukosa tumaini, hasira na uraibu.

Madhara ya kimwili. Kukosa usingizi, kuathirika kwa mpangilio wa kula.

Athari za kitaaluma. Ushiriki hafifu darasani, utoro, kuacha shule, kupungua kwa ufaulu kitaaluma, kukosa umakini katika kazi za shule na kutojiamini.

Athari za kitabia na kijamii. Kuwakwepa marafiki au matukio ya kijamii, matumizi ya madawa ya kulevya, kupoteza hamu ya kufanya alichozoea kufanya, kuepuka kuingia mtandaoni au kutumia vifaa vya kidijitali, matatizo ya uhusiano na marafiki au wanafamilia, kuonyesha tabia mbaya na kutumia lugha isiyofaa.

Wazazi na walezi wanaweza kufanya nini kusaidia watoto?

Ijapokuwa hakuna kanuni moja ya kuwalinda watoto na kuwaweka salama mtandaoni, zifuatazo ni baadhi ya dondoo muhimu ambazo wazazi wanaweza kutumia ili kusaidia na kuwalinda watoto mtandaoni.

- **Jenga uhusiano mzuri na mtoto wako kuhusu matumizi ya TEHAMA.** Mzazi mtie moyo mtoto na kumuelimisha kuhusu matumizi sahihi ya mtandao na usimtishie hata kama utabaini anafanya makosa kwenye matumizi ya mtandao. Hii itamsaidia mtoto kukuza uaminifu na kufichua mapema hali yeyote ya hatari katika matumizi yake ya mtandao na kumpatia usaidizi stahiki.

- **Anza kuzungumza na mtoto wako kuhusu teknolojia katika umri mdogo.** Hakuna umri rasmi wa kumpa mtoto kifaa au kumwacha atumie mtandao akiwa peke yake. Mzazi au mlezi unamjua mtoto wako vizuri zaidi kuliko mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na kama yuko tayari kuanza kutumia vifaa vya kidijiti kwa kujitegemea au chini ya usimamizi. Kwa hivyo, unapaswa kuanza kuzungumza au kumfundisha mtoto wako kuhusu teknolojia na masuala ya usalama mtandaoni mapema kabla ya yeye kuanza kutumia.

- **Kuwa tayari kufuatilia shughuli zake mtandaoni.** Kulingana na umri na kiwango cha mtoto cha ujuzi wa kidijiti, unatakiwa kuwa karibu wakati mtoto anapotumia mtandao. Hii haitamwonesha mtoto kuwa unavutiwa na kile anachofanya tu, bali unaweza kutumia matukio

mnayoyaona kwenye mtandao kama vianzilishi vya mazungumzo kuhusu usalama mtandaoni.

- **Epuka maelekezo marefu kuhusu matumizi ya teknolojia unapowaelekeza watoto.** Jaribu kuwa na mazungumzo mafupi ya kuvutia na ya mara kwa mara ili kuwafanya watoto kuwa na furaha, usalama na ari ya kusikiliza maelezo kuhusu usalama mtandaoni.

- **Jiunge na mwanao mtandaoni ili uweze kumfuatilia katika matumizi yake ya mitandao ya kijamii.** Mtoto wako anapokuwa na kuanza kutumia mitandao ya kijamii, unaweza kukubali kuwa mmoja wa marafiki zake ili kuunga mkono taratibu za usalama mtandaoni. Kumbuka kwamba chochote utakachokiona kwenye jukwaa lake haupaswi kumkalipia bali kitumike kama chanzo cha mazungumzo yenu ya kumnasii.

- **Shirikisha mtoto katika kutengeneza utaratibu wa familia kuhusu matumizi ya vifaa vya kidijiti.** Unashauriwa kuhusisha wanafamilia wote akiwemo mtoto wako katika mchakato wa kuunda sheria za matumizi ya vifaa vya kidijiti. Mjulishe mtoto wako kwamba kinachofaa katika familia yako kinaweza kuwa tofauti kwa wazazi na watoto kutoka katika familia nyingine.

- **Sisitiza watoto kwamba pindi tu wanapotuma au kuweka kitu kwenye mtandao, hawawezi kamwe kukiondoa tena.** Wakumbushe watoto kufikiria picha, video, au ujumbe wa maandishi wanaopanga kuutuma mtandaoni kabla ya kubofya kitufe cha kutuma. Wakumbushe watoto kila mara kwamba kabla ya kutuma chochote mtandaoni, wanapaswa kujiuliza swali hili: JE, MAMA/BABA/MWALIMU/MCHUNGAJI/IMAM ANAWEZA KUONA HILI?

Je, wangefurahishwa na ujumbe wangu? Sisitiza kwamba ikiwa jibu lao kwa swali hili ni HAPANA, basi hawapaswi kuchapisha arafa hizo. Hii ni kwa sababu mara tu ujumbe au picha kama hiyo inapotumwa mtandaoni itasalia hapo na inaweza kuwadhuru baadaye maishani.

- **Pata ujuzi kuhusu mtandao**. Ikiwa ungependa watoto wako wawe salama mtandaoni, fahamu jinsi mtandao unavyofanya kazi. Unahitaji kuelewa nafasi ya kidijiti kama vile jinsi ya kutumia vifaa janja, simu za mkononi, mtandao na kuperuzi tovuti tofauti za mitandao ya kijamii. Hii itakusaidia katika kuwaongoza watoto wako na kujenga mapendeleo yao, uaminifu, na ujasiri wa kutafuta msaada kutoka kwako. Pia itawasaidia kuchagua wanachochapisha, marafiki wanachofuata na jinsi wanavyowasiliana, hata wakati wewe haupo karibu nao.

- **Weka vifaa vyote vinavyohusiana na mtandao vinavyotumiwa na mtoto kwenye nafasi iliyo wazi.** Vifaa vyote vya kielektroniki vinavyohusiana na watoto kama vile kompyuta, kompyuta za mkononi na simu za mkononi vinapaswa kutumiwa na kuchajiwa sebuleni au katika sehemu za wazi zinazoweza kufikiwa na mtu mzima. Haifai kuruhusu watoto kutumia vifaa vya kidijiti katika maeneo ya faragha bila usimamizi wa watu wazima, kwa kuwa wako hatarini kupata madhara ya mtandaoni.

- **Zungumza na mtoto wako kuhusu watu asiowajua mtandaoni.** Kila mara mkumbushe mtoto wako kwamba si kila mtu anayekutana naye mtandaoni anasema ukweli kuhusu yeye ni nani. Sisitiza watoto waepuke kuongeza watu wasiowajua kwenye orodha ya marafiki zao na waepuke kukutana na watu wasiowajua wakiwa nje ya mtandao au ana kwa ana bila kumjulisha mzazi, mwalimu, mtu anayemfahamu au rafiki anayemwamini.

- **Wajulishe watoto wazungumze na mtu mzima wanayemwamini kuhusu matumizi mabaya ya mtandaoni.** Wakumbushe watoto kila mara kuwa makini na kuzungumza na wewe au mtu mzima mwingine yeyote anayeaminika iwapo mtu

fulani anawatumia vibaya mtandaoni au anataka kuzungumza nao kuhusu ngono au jambo lolote wasilolipenda wakiwa mtandaoni. Kila mara mfundishe mtoto wako kukuonyesha picha, ujumbe au maandishi yoyote mabaya au ya kutisha kabla ya kufuta.

- **Mwongoze mtoto kuhusu matumizi yanayofaa na masuala ya faragha mtandaoni.** Mkumbushe mtoto wako aepuke kuweka taarifa zake au za familia mtandaoni kama vile jina, eneo, anwani, barua pepe na namba ya simu ya mkononi. Hizi zinaweza kutumiwa kwa urahisi na wahalifu mtandaoni na kumfikia mtoto au familia alipo.

- **Dhibiti muda ambao mtoto hutumia mtandaoni.** Kadiri mtoto anavyotumia muda mwingi mtandaoni, ndivyo uwezekano wa kuathirika zaidi na hatari za mtandaoni zinavyoongezeka. Kulingana na umri wa mtoto, unapaswa kuweka na kudhibiti muda wa kuperuzi mtandaoni kwa mtoto husika.

Walimu wanaweza kufanya nini kusaidia watoto?

Ingawa shule yako inaweza kuwa na sheria ambazo haziruhusu watoto kuja na simu za mkononi au kompyuta shuleni, lakini uzoefu unaonyesha kwamba watoto wana njia nyingi za kuingia mtandaoni wakiwa nyumbani au shuleni. Jukumu letu kama waelimishaji ni kuwasaidia watoto kutumia fursa zinazotolewa na teknolojia hizi na kuwatayarisha kuwa raia wa kidijiti wanaowajibika.

> Wape watoto fursa za kuongoza mazungumzo kuhusu usalama mtandaoni.

Zifuatazo ni baadhi ya dondoo muhimu kuhusu kile ambacho walimu na waelimishaji wanaweza kufanya ili kuhakikisha kuwa watoto wako salama mtandaoni.

- **Kukuza uhusiano mzuri na watoto kuhusu matumizi ya teknolojia.** Dumisha uhusiano mzuri na watoto katika mazungumzo kuhusu matumizi ya teknolojia. Wafahamishe kuhusu taratibu na sheria za shule kuhusu teknolojia kwa njia itakayowasaidia. Hii itasaidia watoto kukuza uaminifu ili kufichua mambo mabaya wanayokutana nayo mtandaoni na kupata usaidizi unaohitajika.

- **Fikiria kuanzisha mijadala kuhusu matumizi ya teknolojia katika madarasa ya chini.** Kwa kuzingatia kwamba teknolojia na athari hasi zinazohusiana na watoto hazina mipaka, unapaswa kufanya majadiliano ya mtandaoni kuwa mada ya kawaida kwa watoto wa ngazi tofauti ya madarasa. Chagua maudhui yanayofaa kulingana na hitaji na umri wa mtoto.

- **Kuwa tayari kuwasaidia watoto kutumia intaneti.** Watoto, hasa wale ambao wana uzoefu wa kwanza na kompyuta, wanaweza kuhitaji uangalizi wa karibu wa watu wazima katika maabara za kompyuta za shule. Kuwa karibu na kusimamia na kuwakumbusha watoto kuhusu taratibu za usalama mtandaoni katika vyumba vya kompyuta.

- **Epuka maelezo marefu unapozungumza na watoto kuhusu matumizi ya teknolojia.** Panga kutumia mazungumzo mafupi, ya kuvutia na ya mara kwa mara ili kuwaweka watoto wadogo wakiwa na furaha na ari ya kushiriki katika mazungumzo kuhusu usalama mtandaoni.

- **Wape watoto fursa za kuongoza mazungumzo kuhusu usalama mtandaoni.** Waruhusu watoto kuelezea uzoefu wao mtandaoni kulingana na kile wanachofanya mtandaoni, tovuti wanazofungua, programu wanazotumia na watu wanaowasiliana nao mtandaoni kunaweza kuwasaidia walimu kuelewa maisha ya kidijiti ya watoto. Hii itasaidia afua stahiki za kusaidia watoto. Epuka kutaharuki na usichukie sana mtoto anapotoa uzoefu wake wa mtandaoni.

- **Andaa miongozo ya shule kuhusu usalama mtandaoni.** Shirikisha watoto katika mchakato wa kubuni miongozo au taratibu mahususi shuleni au darasani kuhusu usalama mtandaoni na matumizi ya vifaa vya kidijiti. Miongozo hii inapaswa kuwa katika lugha rahisi ya kueleweka. Kushirikisha watoto katika mchakato wa kuandaa miongozo na taratibu za ukatili dhidi ya watoto mtandaoni shuleni itaongeza umiliki na uwajibikaji. Hakikisha miongozo hii inafanyiwa mapitio ya mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko ya kidijiti duniani.

- **Elewa jinsi mtandao unavyotumika.** Unahitaji kuwa na elimu ya kidijiti wewe mwenyewe ili kuwasaidia watoto. Unapaswa kupata maarifa mapya katika nafasi ya kidijiti kama vile jinsi ya kutumia mtandao, vifaa janja, simu za mkononi na jinsi ya kuperuzi tovuti mbalimbali. Hii itaboresha imani na uaminifu wao kutafuta usaidizi kutoka kwako.

- **Wakumbushe watoto kuzungumza nawe au mtu mzima mwingine wanayemwamini.** Wafahamishe watoto kwamba wanaweza kupata usaidizi kwa mtu mzima mwingine wanayemwamini ili kupata usaidizi ikiwa mtu fulani anataka kuwafanyia ukatili mtandaoni. Kila mara wajulishe watoto kuweka rekodi ya nakala ya picha, ujumbe au maandishi ya vitisho kama ushahidi kabla ya kuzifuta.

- **Wafundishe watoto kutumia nywila thabiti kwenye vifaa vya kielektroniki.** Wafundishe kila wakati kuepuka kutoa nywila kwa watu wengine isipokuwa wazazi inapohitajika. Sisitiza watoto kufunga akaunti zao kila wanapotoka kwenye vyumba vya kompyuta au kuacha kutumia kifaa.

- **Wafundishe watoto kuhusu faragha kwenye mtandao.** Waongoze watoto jinsi ya kutumia nyenzo za faragha mtandaoni ili marafiki wao pekee waweze kuona taarifa zao wanazoweka mtandaoni. Pia, unapaswa kuwakumbusha watoto kuepuka kutoa taarifa za kibinafsi na za familia, kama vile jina kamili, eneo, anwani, barua pepe, jina la shule, nambari ya gari na nambari ya simu ya mkononi, kwa watu wasiowajua mtandaoni kwa sababu wanaweza kutumia taarifa hiyo kutambua walipo na kuwadhuru.

- **Wafundishe wafanyakazi wote wasio walimu kuhusu ukatili wa watoto mtandaoni.** Ili kuongeza ufahamu wa watu wengi shuleni kupata uelewa wa ukatili wa mtandaoni, walimu na wafanyakazi wote wasio walimu wanapaswa kupewa mafunzo mara kwa mara kuhusu usalama wa watoto mtandaoni.

- **Waongoze watoto kufahamu vipengele muhimu vya kiusalama mtandaoni.** Kuwa na ujuzi wa vipengele muhimu vya usalama kwa watoto mtandaoni. Fanya mapitio ya kimsingi ya vipengele hivyo kabla ya kuwaelekeza watoto.

Kwa maelezo zaidi na kutoa taarifa unaweza piga simu isiyo na malipo ya msaada ya watoto:

116

Vyanzo vya Taarifa

KIMATAIFA

1. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (UN-CRC) 1989 (Ibara ya 13, 17 na 34)
2. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa 1990. (Ibara ya 15, 16 na 27)
3. Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030). Lengo nambari 16.
4. Ajenda ya Afrika ya Ustawi wa Mtoto (2040). Kifungu cha 7

KITAIFA

1. Sera ya Maendeleo ya Mtoto 2008 (Sura ya 5 (c)
2. Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) (2017/ 18-2021 / 22)
3. Sheria ya Mtoto SURA YA 13
4. Kanuni ya Adhabu SURA 16
5. Sheria ya Mawasiliano ya Kielektoniki na Posta ya Mwaka 2010
6. Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015.

Baadhi ya rasilimali za kuaminika ni kutoka kwa tovuti zifuatazo:

1.	Taarifa ya Utafiti wa *Disrupting Harm* Tanzania 2021	https://www.end-violence.org/sites/default/files/2022-03/DH_Tanzania_ONLINE_final_revise%20020322.pdf
2.	Kitengo cha Ulinzi na Usalama wa Mtoto UNICEF	https://www.unicef.org/tanzania/what-we-do/child-protection
3.	Kituo cha Rasilimali za Mtoto cha Afrika	https://toolkits.childonlineafrica.org/
4.	Tovuti ya Mradi wa *Global Kids Online*	http://globalkidsonline.net/

unicef
for every child